
# Funguo Tano
# Za Kuelekea Kwenye
# Uhusiano wa Kina Zaidi
# Na Bwana




## *Ujumbe kwa ajili ya Bibi Arusi wa Kristo*

*Paul D. Norcross*

**Kingdom Faith Ministries International, Inc.**
PO Box 725 * Charlemont, MA 01339 * USA

© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

*© Copyright 2004, 2007 – Paul D. Norcross*
Haki zote zimehifadhiwa. Kunakili maandiko haya kwa manufaa ya ya kibiashara au faida hakuruhusiwi isipokuwa kwa ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwandishi. Nukuu fupi za sentensi chache zikitumika kwa ajili ya matumizi binafsi yasiyo ya kibiashara zikitumika kwa ajili ya kujifunza mtu binafsi au kikundi au mapitio ya kitabu inahimizwa kikamilifu na hakuna haja ya ruhusa ya kimaandishi inayotakiwa kwa matumizi kama hayo.

Maandiko Matakatifu yote yanatoka kwenye Tafsiri ya King James labda kama imeonyeshwa vinginevyo. Matumizi ya herufi ndogo kwa rejea za shetani ni makusudi; yuko chini ya miguu ya wale ambao wanaongozwa na Roho wa Mungu aliye hai.

Kimechapishwa na:

**Kingdom Presence Publishing**
**S. L. P 725**
**Charlemont, MA 01339**
**USA**

Tovuti: http://www.KingdomFaithMinistries.Org


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

# *Funguo Tano Za Kuelekea Kwenye Uhusiano wa Kina Zaidi Na Bwana*

## *Ujumbe kwa ajili ya Bibi Arusi wa Kristo*

*Dr. Paul D. Norcross*

### *Toleo*

*Kwa Mhudumu wa hekalu, Bwana wetu wa thamani, Yesu Kristo, na kwa Bibi Arusi Wake, akitokea kwenye kila taifa na kila lugha kwenda kwa Mpenzi wake wa Kwanza.*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

## *Yaliyomo*

*Utangulizi* *5*

*1 Ufunguo wa Kwanza* *7*

*2 Ufunguo wa Pili* *13*

*3 Ufunguo wa Tatu* *16*

*4 Ufunguo wa Nne* *20*

*5 Ufunguo wa Tano* *24*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

# Utangulizi

## …*kwamba wawe na umoja, kama na sisi tulivyo na umoja*

Ikiambatanishwa ndani sana katika kila nafsi ni hamu ya kuwa wamoja na Baba yetu wa mbinguni. Tumeumbwa kwa ajili ya utukufu wake, na kupitia ushirika wa karibu na Yeye, ile hamu ya haraka ya mioyo yetu kwa ajili ya umoja na Muumba wetu inatoshelezwa. Hamu ya kutambulika, kutafuta ile maana, na ile hamu ya kusudi linalosukuma kila nafsi yetu, lakini haipati utoshelevu mpaka kila mmoja amemkumbatia Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu, Mjenzi Mkuu wa kusudi letu.

Simama na umtambue Yeye. Yumo katika pumzi yetu inayofuata. Huchochea kamba za furaha na amani pamoja na kila moyo kutoka kwenye kikombe Chake. Kuna uzima kuvuka upeo wa macho yetu, na utimilifu wa shauku nyetu ya kibinadamu kupita fahamu zetu. Unakaa katika Roho wa Mungu aliye hai, anayewafikia wote ambao watatulia na kufikiria njia zake zilizo juu kuliko za kwetu, na mawazo yake ya kina zaidi kuliko ya kwetu. Tunatulia ili tumjue Yeye. Tunatuliza nafsi zetu ili kusema naye. Tumekuwepo hapo tukisikiliza majibu yake ya utulivu. Tunashughulika ili kuingia katika pumziko Lake, ambalo linapatikana tunapotembea katika utulivu wa siku pamoja Naye. Hakuna mpaka kwenye dunia yake. Hakuna mpaka unaomzuia Yeye. Alituumba kwa ajili ya ushirika pamoja Naye, lakini akaturuhusu tumtafute Yeye kwa imani. Jinsi gani anavyotamani kutuvuta tuwe karibu naye! Jinsi gani anavyotafuta ulimwengu wote moyo ulioiva, tayari kwa ajili ya mavuno ya Bwana. Yeye ni Mmoja. Hutembea juu ya kila roho ya thamani, akingojea matunda ya miaka ya kazi ya uvumilivu, na kuwekeza kunakoendelea kwa upendo Wake.

Pole pole kando ya maji ya utulivu, huihuisha nafsi zetu.[1] Huponya kila ugonjwa, na kuutia nguvu kila moyo. Huzihuisha roho zetu, akingojea utayari wetu wa kuelekeza moyo wetu kwenye masafa Yake. Huwategemeza, huwainua, na kushirikiana na wale walio tayari kushusha nyavu zao kwa kutii ushauri Wake. "Je! Wanipenda?" Hunipeleleza tena na tena. "Je! unaweza kukawia na kuongea pamoja nami, na kuniruhusu nikushirikishe moyo wangu. Kila siku akiipeleleza dunia kwa ajili ya mioyo iliyokamilika,[2] Wake ni mwaliko ambao ni mioyo iliyoharibika tu inayoweza kupuuzia – ni ile ambayo imefanywa migumu kwa dhambi, kwa kuta za mafundisho ya imani tofauti, kwa mizizi iliyochimbiwa sana ya kutokutumaini, au kwa kupuuzia tu kutumia muda pamoja na Yeye ambaye tunatakiwa tumpende kuliko vitu vingine vyote.

[1] Zaburi 23:2-3
[2] 2 Nyakati 16:9


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Wapendanao wamezama kila mmoja kwa mwenzake. Hali kadhalika Bwana amezama ndani yetu, kama tukimruhusu. Je! Maisha ni ya muhimu sana kiasi kwamba huwezi kuacha unayofanya leo ili kutumia saa moja pamoja Naye? Pamoja na upendo unaopenya, huiliza kila roho moja kwa moja, kwa uaminifu, kwa shauku –

*...je! hamkuweza kukesha pamoja nami hata kwa saa moja?*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

# 1 *Ufunguo wa Kwanza*

# *Kuelekea kwenye Uhusiano wa Karibu na Bwana*

*Siku moja katika chumba changu cha maombi Bwana aliniambia, "Kitu cha kwanza ninachohitaji kuwafundisha watu wangu kwa kadri wajifunzavyo kuja katika mahali pa uhusiano wa karibu Nami na kusikia sauti Yangu ni kwamba*

**Sitawaacha kamwe wala kuwapungukia.**

*Kwa baadhi hii itachukua miaka kuweza kujenga.*

Bwana aliposema maneno haya kwangu, niligundua kwamba alikuwa amepandikiza mstari wa Biblia unaojulikana (Waebrania 13:5b) katika roho yangu. Ni tofauti kiasi gani hii inavyosikika kuliko ufahamu rahisi wa kiakili !

Kwa hiyo mara nyingi wanaojifunza uwezo wa kuwa watulivu – kutulia vya kutosha katika roho zao kiasi cha kusikia sauti ya utulivu ndogo ya Bwana – wanaanza kufurahia vipindi vya mashirikiano tajiri ya karibu kutoka kwa Bwana.[3] Hufurahi katika ufahamu wa kina na wakusisimua ambao Bwana huwasilisha katika roho zao. Siku inayofuata hutafuta zaidi ya kitu kile kile na huenda hutoka wakiwa wakavu. Kwa nini? Licha ya kutokuwa watulivu kutokana na masumbufu ya kimwili katika nafsi zao,[4] sababu kubwa kuliko zote mara zote huwa mashaka na hofu.

[3] Kijitabu hiki kidogo kinaanza na hoja kwamba kwamba mwandishi tayari amekwisha pitia nyakati za ukaribu wa kina pamoja na Bwana, na anatafuta kukuza mtazamo uleule katika uhusiano huu. Kama huu haujawahi kuwa uzoefu wako, Basi vitabu vitatu kabla ya hiki vya mwandishi vitakuwa vya msaada sana kwako: *Kula Mezani Pa Bwana; Jifunze kusikia sauti ya Bwana, Sauti Juu ya Maji na Mahali pa Siri.* Tafadhali angalia sehemu ya vyanzo vyuma ya kitabu hiki kwa taarifa zaidi.

[4] Nafsi kwa hakika ni tofauti na roho 1Wathesalonike 5:23 na mistari mingine ( kama vile Waebrania 4:12) inasaidia kuweka wazi tofauti kati ya roho, nafsi, na mwili. Kwa ajili ya somo hili roho inaelezewa kama nyumba ya utashi ya kumwitikia Bwana wetu; nafsi ni nyumba ya akili na kufikiri, utashi, na hisia za mwanadamu; mwili hujumuisha mambo kama shauku, tamaa na mihemko isiyotawaliwa ya mwili.


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Mara nyingi pamoja na kukutana kwetu kwa mara ya kwanza peke yetu pamoja na Bwana bustanini, tunachukulia kama matukio tofauti badala ya yalivyokususdiwa kuwa: urafiki unaoendelea, mazungumzo na ushirikiano unaotosheleza. Kujifunza kumruhusu Roho Mtakatifu kuongoza mioyo yetu kando ya maji ya utulivu (Zab 23:2) ni ujuzi wa

- Kujitahidi kuingia katika pumziko lake (Waebrania 3:11-4:16),
- Kujifunza kula miilo kamili ya mkate kutoka mbinguni (Yohana 6:35)
- Kula mezani Pake (Ufunuo 3:20-21)
- na kukaa mahali pa siri pake Aliye juu (Zaburi 91:1).

Hizi ni mbinu za kujifunza. Ni zile ambazo Paulo licha ya mafunzo yake yote miguuni pa Gamalieli, alitenga miaka kumi na saba iliyofuata ya maisha yake baada ya kukutana na Yesu njiani akienda Dameski.[5]

Lakini ni kwa jinsi gani hofu na mashaka huingia ili kuzuia mwendelezo wa kusikia sauti ya Bwana, kwa nini ni lazima kujua (kama ni maarifa ya ufunuo yasiyohamishika badala ya maarifa tu ya kiakili) kwamba Bwana kamwe hatatuacha wala hatatupungukia (Waebrania 13:5b)?

Kinachotokea mara nyingi kwa kadri tunavyotafuta kukutana na Mfalme, ni kwamba huwa tunasahau kuingia malangoni Mwake kwa kushukuru, na nyuani mwake na sifa (Zaburi 100:4). Tukisha kujitahidi kuingia bila kujiandaa (mara nyingi pamoja na mawazo yaliyojaa, usumbufu au manung'uniko), huwa tunashindwa kuunganishwa na Bwana kwa kina cha kutosheleza shauku ya mioyo yetu. Huwa tunalinganisha hali hiyo na kipimo cha furaha yetu wakati uliopita katika uwepo wake na kugundua kwamba si tu tunapungukiwa bali kuhukumiwa.

“Nina shida gani? Bwana yuko wapi? Je! Hapendi kuongea nami tena? Je! Ni kitu gani ambacho nimekosea?”

Mwitikio wetu wa kibinadamu wa kushindwa kurudia ukaribu wa awali pamoja na Bwana ni hofu. Bado hatuko salama katika ufahamu wetu wa upendo Wake. Tunahofia upungufu wetu, na hivyo huwa tunakutana na upungufu juu ya uhusiano wetu tunaojaribu kuujenga. Hili linakuwa shaka binafsi juu ya kustahili kwetu,au kutamani kwetu. Kama muunganiko wetu Naye si wa karibu kama ule wa awali, huwa tunafadhaika kama tumetenda dhambi au la, na tunajiuliza kama Atasema nasi tena au kwa kina cha jinsi hiyo.Kujizingatia binafsi (aina ya kiburi) kunachukua nafasi ya unyenyekevu unaotakiwa na imani ambayo ni lazima ili kujenga na kutegemeza muunganiko wa karibu.

Hali ya kihisia ya kuwepo na kutokuwepo inaweza kuwa tabia ya kutuunganisha kwa kina pamoja na Bwana. Maendeleo katika uhusiano wetu yanakuwa mtindo hadi tunapoteza hofu,mashaka,au shauku na kile kinachotuelekeza kwenye: kutokuwa na imani katika kudumisha upendo Wake na kutamani Kwake kuongea nasi.Je si imani ndio

[5] Wagalatia 1:15-2:10


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

inayompendeza Mungu (Waebrania 11:6), na huleta thawabu kwa wale wamtafutao kwa bidii?

Kwa nini mara nyingi huchukua miaka kujenga ujasiri na muendelezo katika kusikia ufunuo kutoka kwa Bwana? Ni kwa sababu tu wazito katika kujifunza ukweli huu: Bwana hutaka kuongea na wewe zaidi kuliko hata unavyotaka kuongea Naye Analazimika kumsaidia kila mtoto kujifunza kwamba kamwe Hatawaacha wala hatawapungukia. Na lazima wajifunze hili na roho zao, kama hazina iliyoandikwa mioyoni mwao kwa Roho Matakatifu, siyo kwa akili zao.

Lazima tukumbuke kuwa kusudi la msingi la kuzunguka miaka arobaini jangwani lilikuwa kuwawezesha Wasraeli kujifunza namna ya kuishi kwa kusikia sauti ya Bwana (Kumbukumbu 8:1-3). Yoshua 5:6 inatueleza kuwa kushindwa kufanya hivyo ikiwa ndio sababu ya kutoweza kutoka jangwani wakiwa hai.

*Kumbukumbu 8:1-3*
*Amri hii ninayokuamuru leo mtaishika kuitenda, mpate kuishi na kuongezeka, na kuingia katka nchi ile ambayo BWANA aliwaapia baba zenu;nanyi mtaimiliki.Nawe utaikumbuka njia ile yote BWANA Mungu wako,aliyokuongoza miaka hii arobaini katika jangwa , ili akutweze,kukujaribu, kuyajua yaliyo moyoni mwako, kwamba utashika amri zake, au sivyo*
*Akakutweza akakuacha uone njaa, akakulisha mana, usioijua wewe wala baba zako hawakuijua; apate* ***kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu,bali huishi kwa kila neno litokalo katika kinywa cha BWANA***.

*Yoshua 5:6*
***Kwa kuwa wana wa Israeli walitembea muda wa miaka arobaini jangwani hata hilo taifa zima, yaani, watu waume waendao vitani, waliotoka Misri, walipokuwa wameangamia; kwa sababu hawakuisikiliza sauti ya BWANA:*** *nao ndio BWANA aliowaapia ya kwamba hatawaacha waione hiyo nchi, ambayo BWANA aliwaapia baba zao kwamba atatupa sisi; nchi ijaayo maziwa na asali.*

Kama kulikuweko njia nzuri zaidi ya kuwafanya Israeli wajifunze kusikiliza sauti ya Bwana angefanya hivyo. Kwa masikitiko, Israeli kamwe hawakufanya hivyo. Kutokuwa tayari kwao kujifunza kuishi kwa kila neno litokalo katika kinywa Chake (and tunatakiwa kufahamu hivyo kwamba hili ni jambo ambalo mara zote la wakati unaoendelea, kuzungumza kunakoendelea na watu Wake ambao wamejifunza kusikiliza[6]) hakukuwa tu kutokutii kwa bahati mbaya. Kuishi kwa kila neno litokalo katika kinywa Chake na kulitii ulikuwa sehemu ya lazima ili kudumu katika Nchi Ya Ahadi. Bado iko hivyo leo.

---

[6] *Waebrania 12:25-26 – Angalieni msimkatae yeye anenaye* [kama ilivyo neno hili wakati unaoendelea katika Kiyunani, yaani "yeye anayenena"]. *Maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyewaonya* [yaani "yeye anayenena"] *juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye atuonyaye* [yaani "yeye anayenena"] *kutoka mbinguni: Ambaye sauti yake iliitetemesha nchi wakati ule: lakini sasa ameahidi akisema, Mara moja tena nitatetemesha si nchi tu, bali na nchi pia.*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Kujifunza kuishi kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu ni kwa lazima kwa waamini kudumu leo kama ilivyokuwa kwa Israeli. Ni nchi yetu tu ya ahadi imebadilika. Bwana huwa habadilishi makusudi yake au njia kwa ajili ya ushindi![7] Waebrania sura ya 3 na 4 inazungumza juu ya nchi yetu mpya ya ahadi ya pumziko la kiroho, na zinarudia ukweli huu si chini ya mara tatu:

*Waebrania 3:7 – 4:11*
***Kwa hiyo (kama anenavyo Roho Mtakatifu, leo, kama mtaisikia sauti yake,***
***Msifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha, siku ya kujaribiwa katika jangwa:***
*Hapo baba zenu waliponijaribu, wakanipima, wakaona matendo yangu miaka arobaini.*
*Kwa hiyo nalichukizwa na kizazi hiki, nikasema siku zote ni watu waliopotoika mioyo hawa; hawakuzijua njia zangu.*
*Kama nilivyoapa kwa hazira yangu, hawataingia rahani mwangu.) Angalieni, ndugu zangu, moyo mbovu wakutoamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai.*
*Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapoi leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho;*
***Hapo inenwapo, Leo kama mtaisikia sauti yake, msiifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha.***
*Maana ni akina nani waliokasirisha, waliposikia: si wale wote waliotoka Misri wakiongonzwa na Musa?*
*Tena ni akina nani aliochukizwa nao miaka arobaini? Si wale waliokosa, ambao mizoga yao ilianguka katika jangwa?*
*Tena ni akina nani aliowaapia kwamba hawataingia katika raha yake ila wale walioasi?*
*Basi twaona ya kuwa hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao.*
*Basi, ikiwa ikalipo ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.*
*Maana ni kweli, sisi nasi tumeubiriwa habari njema vile vile kama ha. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa wao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia.*
*Maana sisi tulioamini tunaingia katika raha ile; kama vile alivyosema, kama nilivyoapa kwa hasira yangu hawataingia rahani mwangu; ijapokuwa zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.*
*Kwa maana ameinena siku ya saba mahali fulani hivi, Mungu alistarehe siku ya saba, akaziacha kazi zake zote;*
*Na hapo napo, Hawataingia rahani mwangu.*
*Basi, kwa kuwa neno hili limebaki kwamba wako watu watakaoingia humo, na wale waliohubiriwa habari ile zamani, walikosa kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao:*
*Aweka tena siku fulani, akisema katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii,* ***Leo; kama ilivyonenwa tangu zamani, Leo kama mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu.***

[7] *Malaki 3:6a – Kwa kuwa mimi, Bwana, sina kigeugeu;…*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

*Maana kama Yoshua angalkiwapa raha, asingaliinena siku nyingine baadaye. Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu.*
*Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake. Basi, tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.*

Mchakato wa kujifunza kusikia sauti ya Bwana kwa wazi, ujasiri, na kwa kuendelea unahusika kwa kila kitu katika kuujenga moyo mwororo kwa ajili Yake. Kwa njia nyingine, sababu ya watu wengine kumsikia Mungu vizuri na wengine hawafanyi hivyo ni ugumu wa moyo. Ugumu wa moyo huja kutokana na dhambi kama kiburi, kupuuzia na ujeuri. Je! Tunamambo kama hayo maishani mwetu? Tunaweza kuanza kwa kuiliza wenyewe ni mara ngapi tunatulia mbele Yake kusikiliza kwa kile ambacho anataka kutuambia?

Mungu aliona inafaa kurudia onyo hili mara tatu (juu ya ugumu wa moyo kama kizuizi cha kusikia sauti yake) katika mistari ya awali katika Waebrania, ambayo yote ilinukuliwa kutoka Zaburi 95, kwamba moyo mgumu (hasa moyo wa ujeuri na ukaidi) unawazuia watu wake kusikia sauti Yake.

Huu ni ujumbe wa wazi kwa kila kizazi! Mlango ambao hakuna mtu anaweza kuufungua na hakuna mtu anaweza kuufungua,[8] ni huu mlango wa ukaribu na Bwana baada ya mtu kuupata ufunguo kupitia Roho Mtakatifu. Huja kutoka kwenye kujifunza kutuliza moyo polepole, katika unyenyekevu wa peke yake. Huja kutoka kujifunza kufungia nje kelele za nafsi iliyosumbuliwa, na hivyo kumwezesha kusikiliza minong'ono ya Roho wa Bwana.

Kwa wale wanaopitia milango ya unyenyekevu na upole, na wale wanaofuata kula mana kutika mezani pa Bwana kila siku, tabaka za miaka ya ugumu hulainishwa mara nyingi haraka sana. Tabaka baada ya tabaka, kile ambacho hakikutakaswa na si safi kwa upole husafishwa katika maneno ya *rhema* ambayo Bwana hutoa kumsafisha bibi harusi, kanisa Lake la thamani.[9] Lisilo na ila, lisilo na waa wala kunyanzi, kila mwamini hukua na kubadilika ili kufanana na Mpendwa wetu, Mpenzi wetu wa kwanza.[10]

Kwa nini mchakato huu mara nyingi huchukua miaka? Je! Hii haivuki mipaka? Kwa huzuni, hapana. Mara nyingi huchukua miaka si tu kumsikia Bwana mara chache, lakini kutafuta na kuishi kwa kila neno litokalo kinywani mwake kila siku. Kwa bahati mbaya, wachache wako tayari kwenda arabuni kama Paulo alivyofanya, kwa weak kando kila

---

[8] Ufunuo 3:7; Isaya 22:22
[9] Waefeso 5:25-27 – *Enyi waume, wapendeneni wake zenu kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake;* ***ili makusudi alitakase kwa maji katika neno*** [rhema, yaani maneno yaliyotamkwa kutokana na ufunuo wa kusikia sauti ya Kristo], *apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila waka kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisolo na mawaa.*
[10] 2 Wakorinto 3:18 – *Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji tukiurudisha utukufu wa Bwana kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo toka utukufu hata utukufu kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

kitu katika maisha ili kujenga urafiki huu wa binafsi na ujasiri pamoja na Bwana. Ndicho kile ambacho Bwana alimaanisha aliposema “nifuate.”

Katika rehema Zake Baba aliwapa watu Wake miaka arobaini kujifunza na kutii sauti Yake. Je! bado tuna muda wa namna hiyo? Je! tamaa zetu za kufanya tumjue zinaweza kuhamasishwa kwa kuacha shughuli zetu na kumfuata Yeye hata penye maji ya utulivu ya uwepo Wake kila siku? Ni jinsi gani anavyotamani kuwa pamoja nasi, na furaha ya kuonyesha kwamba kamwe hatatuacha wala hatatupungukia, kwa sababu

*…umenishangaza moyo…*

*Wimbo Ulio Bora 4:9a*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

# 2 *Ufunguo Wa pili Kuelekea Kwenye uhusiano wa ukaribu Na Bwana*

*Miezi kadhaa baadaye yalikuja maneno haya.Kama vile kuendelea katikati ya sentensi,Bwana akasema, "na jambo pili ninaliohitaji kuwafundisha watu Wangu ambao wanajifunza kuingia kwenye uhusiano wa karibu na Mimi na kuisikia sauti Yangu ni hili*

**Ninapendezwa nao wanapofanya hivyo"**

Mara nyingi moyo wa Kikristo kwa kutamani hudhani kuwa siku moja, Bwana ataangalia moja kwa moja machoni mwetu na kutuambia, "Vema mtumwa mwema na mwaminifu." Tunatamani kuwa wa kupendeza machoni Pake,na kujua utimilifu Wake, mkumbatio Wake wa kukubali na uthibitisho.

Tunaweza kujua hasa uthibitisho wa namna hiyo, na kuujua sasa! Tuanweza kufurahia ushirika Wake kwa karibu na binafsi na kila siku! Anapendezwa sana ndani yetu tunapotafuta kwanza ufalme wa Mungu, na haki Yake. Na ni nini kutafuta kwanza ufalme wa Mungu?

Ufalme wa Mungu ni uwepo Wake. Kila kwa mfano, mifano ya Bwana Yesu inapozunguzia, ufalme wa Mungu au ufalme wa mbinguni, inarejea kwenye uwepo wa Mungu na uwepo wa Mfalme.[11] "Ufalme uje hapa duniani kama huko mbinguni" inarejea kwenye uwepo wa Mungu na uwepo wa Bwana ukija duniani kwenye mioyo yenye

[11] Msomaji anatiwa moyo kusoma Injili zote kwa upya, na kuchunguza mafundisho ya Yesu juu ya ufalme. Kwa ufahamu wa haraka, soma Mathayo 13, na kutambua kwamba kila "ufalme" unaporejewa, inazungumzia uwepo Wake. Hivyo uwepo wa Bwana ni hazina katika shamba,na mwenye busara atauza vyote ili alinunue. Uwepo wa Bwana ni ile punje ndogo ya haradali inayokua na kuwa mti mkubwa wenye kivuli na unawasitli wote wanaokuja chini yake. Uwepo wa Bwana ni kama chachu ndogo ambayo taratibu inachachua donge zima. Je inafanyanini kwa donge lote? Je uwepo wa Mungu unafanya nini katika mwili wa Kristo? Unasababisha mwili wote kuamka! Uwepo wa Mfalme ulikuwa ndio ujumbe ambao Yesu alikuja kuleta. Alikuja kuhubiri injili ya ufalme, injili ya uwepo Wake.


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

kupokea na yenye njaa ambayo iko tayari kupokea uwepo Wake kama mahekalu ya Roho Mtakatifu. Mbele ya uwepo kuna furaha tele.

Musa alipoomba kuuona utukufu wa Mungu. Mungu aliitika kwa uwepo Wake (Kutoka 12). Utukufu Wake ni uwepo Wake! Adamu na Hawa walipojificha kutoka uwepo Wake, ilikuwa ni sauti Yake iliyoufunua ukaribu Wake (Mwanzo 3:8). Ufalme wa Mungu umo ndani yenu (Luka 17:20, 1Wakorintho 4:20, Warumi 17:5) unahusu uwepo wa Mungu ambao unaweza kupaliliwa na wale walio tayari kuchukua muda kutengeneza uhusiano wa karibu namna hiyo Naye.Uhusiano huu unakuzwa kupitia kujifunza kusikia sauti Yake.

Mfalme Daudi alilielewa hili vizuri. Anaitwa mtu wa moyo wa Mungu[12] katika Maandiko Matakatifu hususan kwa sababu ya uhusiano alioutengeneza na Mungu. Je huu ndio moyo wako pia? Je utafikiria kwenda Arabuni kuupata?[13]

*Zaburi 27:4, 8*
*Neno moja nimelitaka kwa BWANA nalo ndilo nitakalolitafuta, nikae nyumbani mwa BWANA siku zote za maisha yangu. Niutazame uzuri wa BWANA na kutafakari hekaluni mwake.*
*Uliposema, nitafuteni uso wangu, moyo wangu umekwambia, BWANA uso wako nitautafuta.*

*Zaburi 84:2, 10*
*Nafsi yangu imezionea shauku nyua za BWANA: naam na kuzikondea. Moyo wangu na mwili wangu vinamlilia Mungu aliye hai. Hakika siku moja katika nyua zako ni bora kuliko siku elfu. Ningependa kuwa bawabu nyumbani mwa Mungu wangu, kuliko kukaa kwenye hema za uovu.*

Hivyo Bwana anasema kuwa anapendezwa sana na wale wanaotafuta kusikia sauti yake, hukuza uhusiano mazungumzo ya binafsi ya karibnu na Yeye, hata kwenda arabuni (au mahali popote pa kujitenga) kwa kadri kulivyo kwa lazima ili kupata uhusiano binafsi wa kina na Yeye. “Ninapendezwa sana na wewe mwanangu. Napendezwa sana na wewe mwanangu wa kike.” Ni msisimko kiasi gani moyoni mwetu kusikia maneno ya namna

[12] *Matendo 13:22 Na alipokwisha kumwondoa huyo, akamwinua Daudi awe mfalme wao ambaye alimshuhudia akisema, Nimemwona* ***Daudi*** *mwana wa Yese,* ***Mtu anayeupendeza moyo wangu, atakayefanya mapenzi yangu yote.***

[13] Mtume Paulo alikuwa maarufu kati ya watu wa rika lake katika shule ya Gamalieli. Alifanikiwa katika mambo mawili, mwanafunzi aliyejua Maandiko vizuri na pia mtesaji mwenye shauku wa Wawakristo. Hata hivyo aliposhuhudiwa na Bwana Yesu Kristo njiani akienda Dameski, hakuwasiliana na wasomi wa Kibiblia au nyama na damu. Lakini kwa hakika aliwasiliana na mtu fulani. Huyu mtu fulani alikuwa ni Bwana Yesu Kristo. Paulo alitumia miaka kumi na saba iliyofuata shambani uarabuni. Je! Alifanya haya ili kujifunza zaidi Biblia, hapana. Alifanya hivyo kujifunza zaidi juu ya Yesu, yule ambaye binafsi alimwita aingie kwenye huduma. Hazina hii katika sahamba, Paulo aliuza vyote kuinunua. Pamoja na kazi hiyo kumalizika, Bwana alifungua mlango kwa ajili ya huduma yake. Mpendwa, umekwishaembelea uarabuni wako wa kiroho na kukuza uhusiano wako na Yesu?


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

hiyo kutoka kwa mpendwa wetu wa upendo wa kwanza! Anapendezwa sana ndani yetu kwa kadri tunavyotafuta uwepo Wake kwanza, na haki Yake.

*Bali utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*

*Mathayo 6:33*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

# 3 Ufunguo wa Tatu Kuelekea kwenye Uhusiano wa Karibu na Bwana

*Miesi kadhaa ilipita, na tena Bwana akaendeleza mazungumzo bila utangulizi, "Jambo la tatu ambalo nahitaji kuwafundisha watu Wangu ambao wanajifunza kuingia mahali pa uhusiano wa karibu na Mimi ni*

**Wafike mahali ambapo siwaiti tena watumwa, bali marafiki."**

Uhusiano na Bwana unaendelea kama ilivyo kuunganishwa na rafiki bora hakutokei mara moja, kadhalika haitokei mara moja na Bwana. Inachukua muda kufahamiana nao; inachukua matukio ya ajabu na uzoefu wa kawaida pamoja. Urafiki si swala la taa inayowaka na kuzima. Ni jambo la kufuatilia. Raha yetu katika ushirika na wengine inaongezeka pamoja na kila kukutana, kila mazungumzo, na kila kushirikishana uzoefu. Kuaminiana kwetu na kueshimiana kwetu kwa ajili ya kila mmoja na kuaminiana kwa pamoja kunaongezeka kwa kadri tunavyohusiana hivyo ndivyo ilivyo na Bwana! Kwa kadri tunavyokua wajasiri wa uhusiano wetu na Yeye, muda wa kuingia kwenye uwepo Wake unapungua. Kama mtoto anayeingia ofisini kwa baba yake bila taarifa, hivyo urafiki wetu unaoendelea unafungua mlango wa ujasiri na imani ya kuingia katika moyo wa upendo wetu wa kwanza kila tunapokaribia.

Mahali ambapo tulizoea kuhitaji muda mrefu wa kusifu magotini petu, na kusafisha madhabahu tukiomba msamaha wa dhambi zetu kabla ya kuingia nyuani mwake kwa ukaribu – yote hayo ili kuandaa mioyo yetu na kutuliza nafsi zetu kwenye kiwango cha lazima cha unyenyekevu na utulivu – sasa kama marafiki kwa haraka tunapita mlangoni kwenda kwenye chumba cha kiti chake cha enzi. Sana kama Esta, tumezoea kukaa mbali na Mfalme isipokuwa wakati tumekaribishwa kuingia. Inachukua muda kuushinda woga wetu. Hatutambui kwamba tunapokuwa katika chumba cha enzi cha mfalme, fimbo yake mara zote hunyooshwa kuelekea kwetu, akitupa mamlaka kamili ya kuziingia nyua zake wakati wote.[14]

[14] Angalia Esta 4:10-5:2


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Tunajifunza kwa wepesi kuvaa joho la nyua zake la haki, badala ya viraka vyetu vya kujifikiria sisi. Tunajifunza kwa urahisi kutoka kwenye malapa yetu ya shauku ya hali yetu ya machafuko ya ndani, na badala yake tuvae viatu vya amani ya kiroho. Tunafika haraka mahali pa kushukuru, na mshangao wa kina, upendo, na raha kwa kuwa tu pamoja Naye. Tunapoteza kumbukumbu za masumbufu ya nafsi zetu, na tunazamishwa katika furaha ya kuyeyuka katika uwepo wake.

Muda wetu wa kuwa pamoja Naye unaongezeka. Tunabeba nira ya urafiki wake, na tunagundua unakuwa mwepesi zaidi kila siku na wa mapumziko zaidi kwa nafsi zetu.[15] Nafasi zetu chache za ukaribu – siku moja hapa, mkutano kule – zinatoa njia ya kukutana kila siku, tukikutana naye katika bustani wakati wa jua kupunga. Kunakuwa sehemu ya maisha yetu. Inakuwa ndiyo hitaji letu kuu. Tunajifunza kazi ya kuingia katika pumziko[16] lake na kugundua kuwa furaha katika uwepo[17] wake.

Aina ya urafiki ambao hutokea ni tofauti mbali na uhusiano wa mtumishi na bwana wake. Martha, alihangaika kuhusu utumishi wote, ingawa ulisifiwa, ulikuwa umejaa moyo wa utumishi. Kweli uliheshimiwa, lakini Martha alipungukiwa na ukaribu ambao Mariamu aliutamani.Alikuwa Mariamu aliyekaa karibu. Ilikuwa Mariamu ambaye alikua kila wakati akiutumia katika uwepo wake. Ilikuwa Mariamu ambaye aliuvuta moyo wa Mfalme wetu kumfufua Lazaro. Na ilikuwa Mariamu ambaye alijifunua wake palew kaburini; siyo Petro, siyo hata Yohana ama lazaro au Martha.Ilikuwa Mariamu ambaye siku zote alitafuta “kile kitu kizuri zaidi,” miguuni pa Bwana.

Je ungependa Bwana kujifunua mwenyewe kwako? Je moyo wako unatamani mahali hapa pa pumziko kando ya Bwana? Kama bado, usiogope. Hii huja kwa kadri unavyosogea karibu. Roho Mtakatifu hufurahia kukuongoza ikiwa hamu yako ni kuongozwa. Hii Ndiyo maana Bwana alimtuma Roho Mtakatifu kwetu: kutuongoza, kutufariji, kutufundisha kumfikia mhudumu wa hekalu,Yesu Kristo.[18] Hakuna kanuni

---

[15] *Mathayo 11:28-30 Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi.*

[16] *Waebrania 4:9-11* **-** *Basi imesalia raha ya sabatokwa watu wa Mungu*
*Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake,kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake.*
*Basi na tufanye bidii kuingia katika raha ile,ili kwamba mtu ye yote asije akaanguaka kwa mfano uo huo wa kuasi*

[17] *Zaburi16:11* **-** *utanijulisha* ***njia ya uzima****;* ***mbele za uso wako ziko furaha tele****: na katika mkono wako wa kuume mna neema ya milel;e.*

[18] *Waebrania 8:1,2* **-** *Basi katika hayo tunayosema, neno lililo kuu ndilo hili tunaye kuhani mkuu wa namna hii,aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni,mhuedumu wa patatifu, na ile hema ya kweli ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu.*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

inayoweza kutolewa kwa sababu Roho Mtakatifu peke yake ana uwezo wa kumwonyesha kilammoja jinsi ya kuingia mahali pa siri pake Aliye Juu.Lakini kwa kila moyo wenye njaa meza ya karamu ya Bwana imeandaliwa.

*Yohana 15:13-15*
*Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi mmekuwa rafiki zangu mkitenda niwaamuruo. Siwaiti tena watumwa kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki; kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa baba yangu nimearifu.*

Hakuna upendo mkuu kuliko huu kuyatoa maisha yetu kwa ajili ya marafiki. Katika mazingira haya Bwana hatatuita tena watumwa. Badala yake kwa kadiri tunavyojifanza kuweka kando miungu yetu ya “shughuli” tunajifnnza kuyatoa maisha yetu kwa kujifunza kutulia na kusikiliza amri zake, kazi zake kwetu. Urafiki haupatikani kwa kutii tu lakini kwa uhusiano wa karibu ambao unauwezesha. Urafiki hujengwa.

*Zaburi 27:8*
*Uliposema, Nitafuteni uso wangu, Moyo wang uumekwambia, BWANA, uso wako nitautafuta.*

Huduma ya yesu ilikuwa huduma ya kusikia na kutii maneno aliyoyapokea kutoka kwa Baba.[19] Hatima ya kutii kwake ilikuwa msalaba, kazi aliyoipokea kwa ufunuo kutoka kwa Baba. Mfumo wa huduma yake uliyopelekea yeye kwenda msalabani ilikuwa pia kusikia katika roho Yake, na halafu kusema yale ambayo Baba alimpa kusema. Kwa njia hii, Baba alitukuzwa, na miujiza ilitiwa nguvu. Tunatakiwa kufanya hivyo leo; ni alama ya mwanafunzi.[20]

Yesu ni kielelezo chetu. Tunaweza kufanya mambo aliyoyafanya na makubwa zaidi kulingana na Yohana 14:12. Kufanya kwa kiwango hiki kimuijiza, lazima pia tuijifunze kusikia ufunuo na kuutii. Nuhu alifanya. Ibrahimu alifanya.Musa alifanya.Na vyo hivyo Anania mdogo alifanya, akimtii Bwana aliposema naye akimtii Bwana Kumwagiza Paulo mtume wa baadaye. Kwa kadri tunavyojifunza kudumu katika eneo hili la kusikia, ujasiri hukua na kufikia kwenye urafiki. Siku inakuja atakaposema, “Wewe si mtumwa tena, wewe ni rafiki yangu.”

Angalia kwamba ilikuwa mpaka wakati wa mwisho wa kumalizia huduma ya Yesu Kristo ndipo hadhi ya wanafunzi wa ilibadilika kutoka kuwa watumwa hadi marafiki. Huu si upendo mdogo, cheo kidogo anachopewa mtu kwa kufahamiana.wanafunzi

[19] *Yohana 8:26 - Ninayo mengi ya kusema na kuhukumu juu yenu;lakini yeye aliyenipeleka ni kweli,**nami niliyoyasikia kwake ndiyo ninenayo katika ulimwengu.***

[20] *Yohana15:7-8 - **Ninyi mkikaa ndani yangu na maneno yangu**(maneno yaliyosemwa) **yakikaa ndani yenu,**ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.**Hivyo hutukuzwa Baba yangu**,kwa vile mzaavyo sana; nanyi **mtakuwa wanafunzi wangu.**.*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

walikuwa pamoja na Yesu katika huduma yake yote; kupiti aklia muijiza, kila kukutana kwenye huzuni na Mafarisayo wenye jeuri, na kupitia kila somo katika imani. Kuanzia kwenye kutuliza bahari hadi kuwalisha watu elfu tano, wanafunzi waliona. Kutoka kampoteza binamu yake Yohana Mbatizaji, na mpendwa wake Lazaro,hadi kumfufua kutoka kwa wafu, na kuwatuma wale thenashara na wale sabini kufanya ishara zile zile,miujiza na maajabu kama alivyokuwa akifanya-wanafunzi walijifunza na kukua.Lakini kupitia haya yote,wale thenashara bado walikuwa hawajawa marafiki.

Lakini katka Yohana sura 14 mpaka 16, waliagizwa tena. Roho Mtakatyifu alitambulishwa kwamba ndiye kiongozi ambaye angekuja kuwaongoza katika kweli yote. Walihimizwa kupenda sana kiasi kwamba wangeweza kutii amri Zake-kwa wote makundi mawili, wale walioelewa wakati ule na wale ambao angeingia ndani ya roho zao kadri ilivyotiririka toka kwenye Chemchemi ya Maji Yaliyo Hai[21] baada ya ufufuo.Haya yote yanaeleweka miongoni mwa marafiki na sio watumwa tu, wa Bwana yesu Kristo.

Lazima tutambue kwamba mchakato wa kuwa marafiki Zake hauwekewi mipaka na Bwana lakini na sisi wenyewe. Kama uhusiano wo wote wa kirafiki ni mara ngapi na kwa muda kiasi gani tunauutumia peke yetu pamoja na Yeye ni jambo la msingi linaloamua maendeleo yetu.Haitoshi kuwa mfuasi,kwa kuwa wengi wao waliondoka kwa Yesu waliposhindwa kushika ulazima wa kuwasiliana naye kila siku kama mana kutoka mbinguni,na kama nyama ya kula na damu ya kunywa (Yohana 6:47-48).

Miaka arobaini ya kuzunguka ulikuwa muda wa kuthibitisha kama Israeli wangebaki kuwa wanyenyekevu an kujifunza kuishi kwa kila neno lililotoka katika kinywa cha Mungu.[22] Ni miaka mingapi lazima mwamini leo hustaajabu kabla ya kujifunza kuwa na mazungumzo ya karibu pamoja na Bwana, na kufanya hivyo kwa uaminifu? Ni kwa muda mrefu kiasi gani mtu anajenga kujitoa kwa mtumishi, kabla ya kuendelea na kuingia kwenye usikivu wa kujitoa kwa ajili ya rafiki.

---

[21] *Yohana 7:37-39* **-** *Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama; akapaza sautgi akisema, Mtu akiona kiuna aje kwangu anywe*
*Aniaminiye mimi kama vile Maamdiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake*
*(Na neno hili alilisema kwa habari ya Roho, ambaye wale wamwaminiyo watampokea baadae; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa).*

[22] *Kumbukumbu 8:2-3* **-** *Nawe utaikumbuka njia ile yote Bwana Mungu wako,aliyokuongoza miaka hii arobaini katika jangwa ili akutweze,kukujaribu,kutajua yaliyo moyoni mwako,kwamba utazishika amri Zake au sivyo.*
*Akakutweza,akakuacha uone njaa,akakulisha kwa mana,usiy0ijua wewe wala baba zako hawakuijua;* ***apate kukujulisha ya kuwa mwandamu haishi kwa mkate tu,bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha BWANA****.*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

# 4 Ufunguo wa nne wa kuelekea kwenye uhsiano wa karibu na Bwana

*Mwaka mmoja au zaidi ulipita kabla ya Bwana kuendelea kunifundisha hatua ya nne,"Nataka kukufundisha kuhusu wabia.Katika ulimwengu wote na kwa karne zotenimekuwa na marafiki wachache sana,lakini hata zaidi nimekuwa na wabia wachache sana sana*

**Mimi naweza kufanya zaidi sana kupitia wabia kuliko ninavyoweza kufanya kupitia watumishi au marafiki."**

Kuwa mbia ni kuwa mmilki mwenza. Wale ambao huingia kwenye ubia nao ni wamilki wenza wa shughuli. Ni biashara ya kifamilia, shughuli ya ufalme. Yule mbia ni mmilki mwenza wa biashara ya ufalme pamoja na BWANA. Pamoja na umilki wenza, yale yote ambayo ni mali ya Bwana pia ni mali ya wabia Wake.Ufalme kwa namna ile ile ni mali ya mbia kama ilvyo ya Bwana. Ufalme ndilo jina la biashara ya kifamilia. Na ubia ni mkuu kuliko urafiki. Je anaweza kukualika kuwa mbia pamoja naye

*Yohana17:21*
*Wote wawe na umoja;kama wewe Baba,ulivyo ndani yangu,nami ndani yako;hao nao wawe ndani yetu ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.*

Tofauti kati ya ubia na urafiki ni kama tofauti kati ya urafiki na utumishi. Mtumishi hufanya matakwa ya Bwana nje ya mamlaka yake.Rafiki hufanya mapenzi ya rafiki wa karibu kwa sababu ya upendo.lakini mbia hufanya mapenzi ya mbia mwenza kutokana na makubaliano ya pamoja. Ni uhusiano wa utendaji ambao umejengwa juu ya kutambua uthamani wa yote mawili uhusiano wa karibu na uaminifu uliothibitishwa wabia hukubaliana pamoja kwanza juu ya nini kinahitajiwa kufanyika katika shughuli ya kifamilia. Wanashirikishana kikamilifu pamoja. Kile ambacho ni mali ya mmoja, ni mali ya mwingine hujifunza kufanya kwa makubaliano kamili mmoja kwa mwingine. Kuhusu shughuli ya Ufalme, wanakuwa wamoja.


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Hivyo mbia na Bwana hahangaiki Halalamiki. Badala yake, wabia hujadidli na kukubaliana, na makubaliano yanapofikiwa,yale yote ambayo ni ya lazima kutekeleza makubaliano hupatikana.[23] Kibali cha Mungu huachiliwa. Hakuna matakwa ya ajabu ajabu,wala shauku ya kimya ya kutokuwa na shukurani kwa hila. Kuna miongoni mwa mambo, kusudi na ujasiri, tumaini na upendo, heshima na kushukuru.kuna ushirikiano wa moyo na akilinkamwe hakuna uhuru au ujanja wa kutambauliwa.

Siyo kwamba ubia huu ni sawa.Lakini Bwana yuko tayari na anaweza kufanya kazi na wale ambao kwao atatiririka nao katika umoja.Hakuna mabishano, shaka wala dhana ya kusumbua maendeleo ya shughuli za Ufalme. Yeye hufanya kazi hii kama vile ni sawa na mbia wake ingawaje ana mchango mdogo wa kutoa.

Ibrahimu alikuwa mbia wa namna hiyo. Mungu alipoonyesha nia Yake ya kuishughulikia miji ya Sodoma na Gomora, ulikuwa uhusiano wake na Yeye (Mungu) uliochochea utayari wa kuingia katika kuuliza, na hata kujadiliiana kinyume na Mungu kuhusu uamuzi Wake.[24] Kama vile ambavyo Bwana amechagua kutofanya lo lote bila kuwajulisha manabii Wake,[25] na kama vile Bwana alivyochagua kumwambia Ibrahimu mpango Wake, kadhalika wabia wanavyofanya pamoja Naye katika Ufalme kutafuta maoni ya kila mmoja wao na kuendeleza mipango yao kwa faida wa kila mmoja wao kwa kukubaliana. Ingawa Bwana kwa urahisi anaweza kufanya kazi bila wale anaofanya ubia nao. Hata hivyo Huchagua kufanya vinginevyo.Hii hufanya siyo kwa sababu anawahitaji. Hufanya ubia kwa sababu anawataka.

"Ufalme wa Mungu umefanana…[26]" ndio msemo wa Bwana unaoelezea yale ambayo hayawezi kushikwa kwa uwezo wa maneno ya kisomi tu, na ambayo hawapewi wale ambao hawamwoni wala hawamsikii.[27] Hivyo Ufalme unaelezewa kwa mifano na misemo ya picha kufafanua tabia yake. Lakini Ufalme ni juu ya uwepo wa Mfalme. Hivyo pia wazo la ubia wa kiroho huharibu maelezo ya kisomi. Lakini katika kupima tabia ya ubia ya Roho Mtakatifu, asili ya ubia wa kiroho wa Bwana inakuwa wazi zaidi.

*Yohana 14:15-21*
*Mkinipenda,mtazishika amri zangu.Nami nitamwomba Baba,naye* ***atawapa Msaidizi mwingine*** [parakletos = mwombeaji,mtulizaji, wakili,mfariji] ***ili akae nanyi milele;****ndiye Roho wa kweli;ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea,kwa kuwa haumwoni wala hamtambui;bali****ninyi mnamtambua,maana anakaa kwenu,naye atakuwa ndani yenu.***

---

[23] *Amosi 3:3 Can two walk together except they be agreed?*

[24] *Mwanzos 18:17-33*

[25] *Amosis 3:7*

[26] *Mathayo 13*

[27] *Mathayo 13:13*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

*Sitawaacha ninyi yatima;naja kwenu.Nami nitamwomba Baba,**naye atawapa Msaidizi mwingine** [parakletos=mwombeaji,mtulizaji,wakili,mfariji], **ili akae nanyi hata milele,**ndiye Roho wa kweli;;ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa hamwoni wala hamtambui;bali ninyi **mnamtambua, maana anakaa kwenu,naye atakuwa ndani yenu**. Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu.Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena bali **ninyi mnaniona**.Na kwa sababu mimi ni hai ninyi nanyi mtakuwa hai.Siku ile **mtatambua** ya kuwa mimi ni ndani ya baba yangu , nanyi ndani yangu, nami ndani yenu. Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda **na kujidhihirisha kwake***

*Yohana 14:26*
*Lakini **huyo Msaidizi,** huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowambia*

*Yohana 15:26*
*Lakini **ajapo huyo Msaidizi,** nitakayewapelekea kutoka kwa Baba huyo Roho w2a kweli, atoakye kwa Baba, yeye **atanishuhudia***

*Yohana 16:7-8*
*Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke;kwa maana mimi nisipoondoka, **huyo Msaidizi** hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu. Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki na hukumu.*

*Yohana 16:13-15*
***Lakini Yeye atakapokuja**, **huyo Roho wa kweli**,**atawaongoza*** [ hodegeo=kuonyesha njia, ongoza,elekeza]***ninyi kwenye kweli yote;kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe,lakini yote atayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.***
***Yeye atanitukuza mimi;kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari.***
*Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba **atatwaa katika yaliyo yangu**, **na kuwapasheni habari***

*Yohana 13:20*
*Amin,amin nawaambieni,Yeye **anipokeaye mtu ye yote nimpelekaye**,**anipokea mimi**, **naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenipeleka.***

Kipawa cha Roho Mtakatifu ni zawadi ya ajabu kuliko zote kwa watoto Mungu. Ni Roho ambaye huwawesha kuwasiliana na Bwana wetu. Kama msiri wetu na mara nyingi mwenza mkimya (kwa kwaida huzungumza wakati tunaomba maoni yake!), Ambaye tumepewa na Bwana Yesu Kristo. Roho Mtakatifu ndiye mbia mkamilifu ambaye huongea tu yale ambayo Bwana humpa Yeye kuongea na sisi. Wao ni wamoja, na kusudi alo ni kutufanya sisi wamoja pia pamoja nao na Baba yetu. Huu ni ubia wa umoja. Huu ni ubia wa wafanya kazi wenza wa ufalme. Hii ni shughuli kamili ya kifamilia.


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Watakatifu wengi hawajui hawaijui nafsi ya Roho Mtakatifu. Lakini Roho Mtakatifu anapotajwa na kushirikishwa kama nafsi, na wakati anapokaribishwa kukumbatiwa katika moyo wa mtu, mara uwepo wake huvamia nafsi yote katika moyo ambao umejitoa kwake. Yeye kamwe huwa haonyeshi uwepo wake kujidhihirisha bila kukaribishwa; Mapenzi yake kamwe hayajitengi na Bwana. Yeye ndiye kipawa cha Bwana Tesu Kristo, Kazi yake ni kuwaongoza watu wa Mungu kuingia kwenye ukaribu wa kina na Bwana, Ambaye ni kweli yote, Jina lake ni Yesu Kristo, Mfalme wa ufame wa Mungu.

Hivyo tunaweza kuja kwenye kumbatio kubwa la upendo wa Baba. Utukufu wa Bwana ndio uwepo wake, na ile shauku ya Roho Mtakatifu kuwezesha utukufu wa Mungu kuongezeka duniani, una kila kitu kihusucho kuongezeka ubia na Yesu Kristo. Ubia wetu unaoongezeka na Roho Mtakatifu hutuongoza kwenye ongezeko la ukaribu wa upendo wetu wa kwanza.

Ngoja. Tulia. Mwombe Roho Mtakatifu akujaze kwa upya. Mruhusu akuongoze kwenye furaha ya uwepo wa Bwana, kwa kuwa katika kuna furaha tele. Haya ni mapito ya maisha[28] yaliyotengenezwa na Bwana na yanatekelezwa na Roho Mtakatifu.[29] Yeye ndiye mbia mkamilifu kutusaidia katika kufuatilia shauku ya mataifa yote,[30] Yesu Kristo!

[28] Zaburi 16:11

[29] Yohana 13:20

[30] Hagai 2:7


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

# 5 Ufunguo Wa Tano Kuelekea Kwenye Uhusiano Wa Karibu Zaidi Na Bwana

*Miezi sita baadaye…….”Hatua ya tano na mwisho nataka kukufundisha wewe ili uwafundishe wengine kuhusu ukaribu na mimini kwamba*

**Ubia mkubwa zaidi kuliko wote uliopo ni Ubia wa Bibi Arusi Pamoja na Bwana Arusi.”**

Hakuna ubia mkubwa kuliko ule bibi arusi na Bwana Arusi[31] wake. Kumpata mwenza sahihi wa kuoa. Kusudi la mtumishi wa Ibrahimu, akitafuta bibi arusi wa kufaa kwa ajili ya mwanae wa pekee wa ahadi, Isaka.

---

[31] Yerusalemu mpya ni nini? Bibi Arusi wa Kristo nin nini? Yerusalemu mpya inatambuliwa katika Maandiko kama yote mawili Mji uliopambwa, pia kama Bibi arusi wa Mwana kondoo (uUfunuo 21:9-10). Ni yote mawili, mahali pa kiroho(kama ilivyoonyeshwa katika Ufunuo 3:12; 21:2,,10-27) na mke wa Mwanakondoo. Ndani yake wamo watakatifu ambao ni hekalu la Roho Mtakatifu (1Wakorintho 3:16-17; 6:19; 2 Wakorintho 6:16; Waefeso 2:21; Ufunuo 3:12) pamoja na Yesu Kristo Mwanakondoo and Bwana Mungu (Ufunuo 21:22). Kama hay yote ni maelezo ya mifano kwa ktu kinachoshangaza na kinaeleza umbile la kibinadamu la kimwili,au yote ni mfano halisi ya ukweli ya uhusiano wetu na Bwana, wazo na kuwepo kwa uhusiano unaofananishwa na Bibi Arusi wa Bwana liko wazi katika Maandiko.

*Ufunuo 19:7-9 na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya MwanaKondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayar. Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing’arayo, safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu naye akaniambi, Andika, Heri walioalikwa karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo. Akaniambia, Maneno haya ni maneno ya kweli ya Mungu.*

*Ufunuo 21:2, 9-10 Nami Yohana nikauona* ***mji ule matakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu,umewekwa tayari, kama Bibi-Arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.*** *Akaja mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vile vitasa saba vilivyojaa yale mapigo ya mwisho, naye akanena nami, akisema* ***Njoo huku, nami nitakuonyesha yule Bibi-Arusi, mke wa Mwana-***


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

Mtumishi alikuwa kwenye utume, na alijitoa kwa kusudi. Alitafuta kwa macho ya Kimungu, na kumthibitisha yule ambaye alikuwa amemchagua. Alijihakikisha mwenyewe kwamba anastahili Rebeka lilikuwa jina lake.Hali kadhalika Roho Mtakatifu anajitafutia bibi-arusi anayefaa kwa ajili ya Bwana wake.

Huyu Bwana ndiye mpenzi wetu wa kwanza ambaye upendo wetu ni mmoja na wa kujitoa. *Ni huyu mpendwa wangu, ni huyu rafiki yangu (Wimbo ulio Bora 5:16b)….Mpendwa wangu ni wangu na mimi ni wake (Wimbo Ulio Bora 2:16a)…Umenishangaza moyo (Wimbo Ulio Bora 4:9a)…*

*Wimbo Ulio Bora 2:10-14*
*Mpendwa wangu alinena, akaniambia, Ondoka, mpenzi wangu, mzuri wang, uje zako,*
*11 maana tazama, kasikazi imepita, Masika imekwisha imekwenda zake;*
*12 maua yatokea katika nchi, Wakati wa kupelea umefika, Sauti ya mwigo husikiwa kwetu*
*13 mtini wapevusha tini zake, na mizabibu inachanua, Inatoa harufu yake nzuri;*
*Ondoka, mpenzi wangu, mzuri wangu, uje zako*
*14* ***Huwa wangu mafichoni mwa jabali, Katika stara za magennge, Nitazame uso wako, nisikie sauti yako, Maana sauti yako ni tamu na uso wako mzuri.***

*Yule Bibi arusi, akiishakujifunza kwamba*

- Mumewe kamwe hataondoka wala hatamwacha
- Kwamba anapendezwa na kuwepo kwake kwa upendo akikutana naye
- Na akiisha kukuza ukaribu wao kutoka kwenye ubwana na utwana mpaka kwenye urafiki wa kujitolea
- Na akiiisha kutamani zaidi akiwa na njaa kwa ajili ya upendo wa kina, na kuonyesha uaminifu wake na kuwa na stahili ya kuaminiwa katika ubia wa shughuli ya kifamilia
- Shauku ya moyo wa Bwana inakuwa kama moto usioweza kuzimwa kwa mbia wake wa kweli kwa milele, Yule Bibi arusi wa kiu yake ambaye atamwakilisha mbele ya Baba ayke, kanisa lenye utukufu,[32] mshirika anayefaa na anayestahili kwa vizazi vyote vinavyokuja.

---

***Kondoo.*** *Akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa mrefu* ***akanionyesha ule mji mtakatifu,Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu,***

[32] *Waefeso* 5:25-27 - *Kwa hiyo kama vile kanisa limtiivyo Kristo, hivyo wake wawe hivyo kwa waume zao katika kila jambo*
*Waume wapendeni wake zenu, kama Kristo alivyolipenda kanisa,akajitoa kwa ajili yake*;
*Ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.

*Ufunuo 21:9b-11*
*…Njoo huku, nami ntakuonyesha yule Bibi-arusi,mke wa Mwana-Kondoo.*
*10 akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akanionyesha ule mji mtakatifu,Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu,*
*11Mwenye utukufu wa Mungu, na mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kito cha yaspi, safi kama bilauri;*

*Ufunuo 22:17*
*Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! naye mwenye kiu na aje; naye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure.*

Wapendwa, njoni na mpenzi wenu wa kwanza. Mruhusuni awalee na kuwafurahisha mioyo yenu kama ninyi mnavyofanya.Ruhusuni upendo wake uwapeleke kwenye kina katika mahali pa ukaribu pa kukaa ambako alienda kuandaa kwa ajili yenu[33] mahali pa siri.[34] Hapa ni mahali pa maandalizi pa Bibi-arusi, na lazima pawe ndiyo haja ya mioyo yetu. Hakuna kitu kingine kinachojalisha zaidi, kwa sababu katika kutafuta kwanza uwepo wa ufalme wa Mungu, atupaye kila hitaji.[35]

Hivyo ni hiki ambacho matakwa ya ulimwengu hayawezi kuzuia, na hayawi kizuizi, sababu au udhuru kwa ajili ya kutokubaliana na udhaifu, kwa kumfuata Mpendwa wetu. Yeye ndiye yote ndani ya yote na katika yote. Yeye ni wetu na sisi tu wake. Kila siku, kwa kuendelea, kwa njia ya Roho Mtakatifu humtumikia Baba, akimtafuta Bibi-arusi kwa ajili ya Mwanae. Hili litakuwa ni lile hekalu lisilotengenezwa kwa mikono, mahali pa mwisho pa mapumziko kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Na akiisha kuonekana na Yeye Bibi-arusi anapata pumziko na utoshelevu kwa milele yote.

---

*Apate kujiletea Kanisa tukufu,lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo bali liwe takatifu lisilo na mawaa*

[33] *Yohana 14:1-3* **-** *Msifahdaike mioyoni mwenu;mnamwamini Mungu niaminini na mimi Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi, kama sivyo ningaliwaambia.Naenda kuwaandalia mahali,nitakuja tena niwakaribishe kwangu* ***ili nilipo mimi, nanyi mwepo.***

[34] *Zaburi 91:1 Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu, Atakaa katika uvuli wake Mwenyezi.*

[35] *Mathayo 6:33 Bali utafuteni kwanza ufalme wake na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*


© 2012 Paul D. Norcross. All rights reserved.